**HOTUBA YA KAIMU KATIBU MKUU OFISI YA RAIS-MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA BW. HAB MKWIZU KWENYE UFUNGUZI WA KONGAMANO LA KWANZA LA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA, TAREHE 17-20 AGOSTI, 2015**

***Katibu Tawala Mkoa wa Arusha,***
***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao***
***Watendaji wa Taasisi za Serikali,***
***Watoa Mada,***
***Wageni Waalikwa,***
***Wana Habari,***
***Mabibi na Mabwana,***

***Habari za asubuhi.***

Awali ya yote, namshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima, afya na nguvu na kutuwezesha kuwepo hapa leo hii. Aidha naushukuru uongozi wa Mkoa wa Arusha hususan Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha ambaye yupo pamoja nasi leo kwa kutupokea katika himaya yake. Tunaamini tuko katika mikono salama na tutaendelea kuwa hivyo kwa siku zote nne za Kongamano hili.

***Ndugu Washiriki,***

Naomba nichukue pia fursa hii kuwakaribisha wote katika Kongamanohili la kwanza la Serikali Mtandao. Ninaamini kwamba, Maafisa Watendaji wakiwemo Maafisa TEHAMA, Mipango,Habari, Utawala na Rasilimaliwatumlioalikwa mpo hapa. Nawakaribisha pia wadau mbalimbali

ambao mmeona umuhimu wa kuhudhuria tukio hili muhimu katika jitihada zetu za utekelezaji wa Serikali Mtandao kwenye Utumishi wa Umma.

Natambua uwepo wa wageni wetu ndugu Tan Kim Leng kutoka Singapore na Dr. Rajendra Kumar kutoka India ambao wanahudhuria Kongamano hili ili kubadilishana uzoefu wa utekelezaji wa Serikali Mtandao. Kama mnavyofahamu, Singapore na India ni mifano ya kuigwa kwenye utekelezaji wa Serikali Mtandao duniani. Ni fursa adhimu kwetu kujifunza kutoka kwao kupitia uwepo wao hapa.

***"Mr. Kim and Dr. Rajendra, I warmly welcome you to Tanzaniafor the 1st e-Government Annual Conference 2015.It is my sincere hope that your stay here though short, willbe as pleasant as possible. We thank you for attending this conference and giving it the weight and importance itdeserves".Nasema karibuni sana.***

Ninapenda kutambua mchango wa wadau mbalimbali ambao wamefanikisha Kongamano hili. Michango yenu ya hali na mali imefanikisha kufanyika kwa tukio hili la kwanza na la aina yake kwenye Utumishi wa Umma. Kipekee ninaomba kutoka shukrani zangu za dhati kwa Mradi wa RCIP,Taasisi za TASAF,TCRA,NHIF na PPF, na Kampuni za COMPUTECH, COPY CATS na ZANTELambao wamefadhili mkutano huu.Ninawaomba muendelee kuona umuhimu wa kusaidia tena jitihada kama hizi kwa vipindi vijavyo.

Aidha, kwa umuhimu wa pekee,naipongeza Wakala ya Serikali Mtandao kwa kwa ubunifu wao wa kuandaa tukio kama hili katika mazingira

magumu ya ufinyu wa bajeti. Awali lilikuwa wazo ambalo hatukuwa na uhakika wa uhalisia kuhusu utekelezaji wake, lakini kwa bidii, uthubutu, mipango na ushirikiano na wadau mbalimbali hili limewezekana na sote ni mashahidi. Nawaasa muendelee kupanua wigo wa washiriki ili Kongamano kama hili liunganishe nguvu za wadau wote kwenye eneo hili la Serikali Mtandao.

***Ndugu Washiriki,***

Kama mlivyoelezwa kwenye barua za mialiko, Kongamano hililinalenga kuwakutanisha wadau wanaohusika na utekelezaji wa Serikali Mtandao ili kujenga uwezo, kuongeza ushirikiano, kubadilishana uzoefu na kujadiliana njia sahihi ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini. Mada za Kongamano hili zitajikita katika Uhusiano wa Maboresho ya Utumishi wa Umma na Serikali Mtandao, Sera, Sheria na Miongozo ya Serikali Mtandao, Usimamzi wa matumizi ya TEHAMA, Miundombinu ya Serikali Mtandao, Mifumo Tumizi na Huduma Mtandao. Pamoja na Mada hizimtapata pia nafasi ya kujadili changamoto mbalimbali zinazokabili utekelezaji wa Serikali Mtandao na jinsi ya kuzitatua.

***Ndugu Washiriki,***

Kongamano hili linaongozwa na kauli mbiu isemayo (kwa tafsiri isiyo rasmi) “***Rasilimali za TEHAMA Zilizowianishwa Zinaboresha Utoaji Huduma kwa Umma kwa Ufanisi”;(Towards Harmonized ICT Recourses for Improved Public Service Delivery).*** Kauli mbiu hii imetokana na ukweli kwamba, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na unaoendelea kufanywa na taasisi nyingi za umma kwenye eneo la

TEHAMA, bado kuna changamoto kubwa za mifumo hii kutokuongea, kutowasiliana na kutobadilishana taarifa (ndani ya taasisi, na kati ya taasisi na taasisi), rudufu ya mifumoambapo kila taasisi inakuwa na juhudi za kipekee katika kusimika na kutumia miundombinu ya TEHAMA ambayo ingeweza kutumiwa na zaidi ya taasisi moja pamoja na changamoto ya mifumo kuwa na viwango vya usimikaji tofauti.

Baadhi ya sababu zinazochangia changamoto hizi ni kukosekana kwa miongozo, kanuni na usimamizi usioridhisha, ukosefu wa watalaamu wa TEHAMA wenye uwezo wa kutosha, misukumo kutoka kwa wafanyabiashara na wafadhili pamoja na uhusiano na uratibu hafifu wa shughuli za TEHAMA ndani na kati ya Taasisi za Serikali.Aidha, katika Kongamano hili, mtajulishwa na pia kubadilishana uzoefu kuhusu hatua zinazochukuliwa na zinazoweza kuchukuliwa ili kuwa na kanuni na miongozo ya usimamizi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA na kuboresha mahusiano na uratibu wa shughuli za TEHAMA Serikalini.

Hatua hizi zitasaidia ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa taasisi za Serikali, hivyo kutoa fursa kwa matumizi ya TEHAMA yatakayorahisisha mawasiliano na utangamano (integration) wa mifumo mbalimbali. Hali hii itaweza pia kurahisisha ukusanyaji, uhifadhi, utumiaji, uhuishaji na ubadilishanaji wa taarifa miongoni mwa taasisi na sekta zote za Serikali

***Ndugu washiriki,***

Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo yenye dhamana ya utekelezaji wa Serikali Mtandao. Hii inatokana na ukweli kwamba Wizara hii ndiyo inayosimamia Utumishi wa Umma. Ninapenda kuwakumbusha kuwa msingi mkuu wa Utumishi wa Umma ni ubora wa huduma zinazotolewa. Katika maboresho ya Utumishi wa Umma eneo la mifumo na sera za kusaidia utendaji kazi (systems and policies to support service Delivery) tulilenga kuwa na mikakati ya kisera na kimfumo ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananachi. Kimsingi tuliazimia kuboresha utoaji wa huduma miongoni mwa taasisi za umma (Government to Government), kati ya taasisi za umma na wananchi (Government to Citizens) na kati ya taasisi za umma na sekta ya Biashara (Government to Business). Utekelezaji wa Serikali Mtandao ulikuwa ni moja ya sehemu muhimu ya maboresho hayo katika eneo hili kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma hizo kwa kutumia TEHAMA.

***Ndugu Washiriki,***

Pamoja na dhamira ya kuboresha utoaji wa huduma, utekelezaji wa Serikali Mtandao unakusudia kufikia malengo ya kuimarisha utawala bora na kuongeza tija na ufanisi katika uendeshaji wa taasisi za Umma kwa kuhakikisha uwepo wa mawasiliano ya haraka, yenye uhakika na salama ndani na kati ya taasisi mbalimbali za Serikali; kuanzia kwenye Wizara, Mikoa hadi ngazi za Halmashauri pamoja na Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, Serikali Mtandao inadhamiria kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali; kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi Serikalini; kuimarisha usalama wa Serikali na raia wake katika karne ya

sayansi na teknolojia kwa kuongeza uwezo wa Serikali kupambana na majanga kwa kutumia teknolojia; kurahisisha michakato ya utendaji kazi katika taasisi za Serikali na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Malengo haya yanatekelezeka kwa kutegemea uimara wa mifumo ya ndani ya Serikali. Kukiwa na mifumo dhaifu, uboreshaji wa huduma zetu kwa kutumia TEHAMA utakuwa mgumu.Tukiwa na mifumo imara, matumizi ya TEHAMA yatatusaidia kuleta tija na ufanisi wa utoaji wa huduma zetu. Kama mtakavyokuwa mnaumbuka, Serikali ilifanya uboreshaji wa mifumo ya utendaji kazi (business process improvement) wakati wa Programu ya maboresho ya Utumishi ya Umma (PSRP). Ni vyema tukatumia fursa ya TEHAMA kuendelea kuboresha mifumo hiyo na pia kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mifumo hiyo ili kuendelea kuimarisha na kuifanya ilete tija na ufanisi uliokusudiwa kwa kuwa maboresho ni zoezi endelevu. Aidha, niwakumbushe kwamba utekelezaji wa Serikali Mtandao ni suala la kisera na kimkakati. Ubunifu wa sera na mikakati ya utekelezaji wa Serikali Mtandao ni jambo la kutazamwa mara kwa mara kulingana na maendeleo yanayopatikana na changamoto zinazojitokeza.

Mwisho, napenda niwakumbushe kuwa mkiwa kama watumishi wa Umma, ni muhimu kutambua kuwa Utumishi wa Umma unaohitajika zama hizi za Serikali Mtandao ni ule wenye watumishi wenye maadili, weledi na ubunifu katika utendaji wao wa kazi; na si Utumishi wa kufanya kazi kwa mazoea au kusukumwa. Hivyo nawaasa tuwe na mitizamo ya kujiendeleza na kufanya kazi kwa bidii ili tuweze kuwa wabunifu katika kutimiza wajibu wetu

wa kila siku kwenye  ofisi zetu. Tukumbuke kuwa Utumishi wa Umma usipotimiza wajibu wake kikamilifu unasababisha huduma zinazotolewa na Serikali kwa Umma kutokidhi viwango tarajiwa hivyo kuifanya Serikali kushindwa kufikia malengo yake ya Kitaifa iliyojiwekea katika kuwahudumia wananchi wake. Ni muhimu wote tukatambua kuwa UTUMISHI WA UMMA IMARA HUJENGA SERIKALI NA TAIFA IMARA.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa mara nyingine tena, nawashukuru nyote pamoja na waandaji wa kongamano hili kwa kunipa nafasi yakufungua Kongamano hili.Nawaomba tujadili mada zitakazowasilishwa kwa uwazi na mapana yake kwa kuwakwa kufanya majadiliano na kubadilishana uzoefu kama tutakavyofanya katika Kongamano ili ni njia muafaka ya  kufikia utekelezaji bora wa Serikali Mtandao kwa manufaa ya Utumishi bora wa Umma katika kutoa huduma kwa ufanisi kwa Umma.

***Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka kwamba mkutano huu umefunguliwa rasmi.***

***Ninakutakieni majadiliano mazuri na yenye tija.***

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA***